

*Shairi lifuatalo liliandikwa na Marehemu Hamidu Rajabu Tambwe mwishoni mwa miaka ya 1960, shairi hili la "Mwanafulani" linazungumzia mapenzi, na linajaribu kumfunda huyo kipenzi "Mariam" kuweza kufuata maadili mema.*

## **MWANAFULANI**

1. **M**auhudi ndiye wewe, nikutakae kwa huba,  
Mke ndiye uwe wewe, wengine kwangu ni miba,  
Mambo yangu yawe nawe, unifariji kwa heba,  
Mola na atujalie, kuishi bila misiba.
2. **A**semayo wako mama, mimi nimesha yashiba,  
Ambaa yenye zahama, uhibu mwenye haiba,  
Acha siache ya mama, ukapatwa na aiba,  
Akhi na tujaaliwe, kuishi bila misiba.
3. **R**afathi zetu na ziwe, kama asemavyo baba,  
Rai zangu ziwe nawe, pasiwepo na miraba,  
Rajimi jikinge nae, uepuke na kuiba,  
Raha na isipotee, tuishi bila misiba.
4. **I**nda uiweke nyuma, ubaki kuomba toba,  
Inapunguza heshima, japo iwe ni kibaba,  
Inadi kwako tavuma, ukapoteza mahaba,  
Ila haya siachie, tukishi bila misiba.
5. **A**u kama ukimbie, hapo alosema baba,  
Ajapo wapi wendee, haya yaweke akiba,  
Asaa uyaelewe, yatakufanya kushiba,  
Ai! huko utulie, tuishi bila misiba.
6. **M**engi sana nimesema, mengine ni ya akiba,  
Maneno mengi si nyama huyali na ukashiba,  
Moyoni yaliyo mema, weka bila ya ghadhaba,  
Mola na atujalie, kuishi bila misiba.

***Hamidu R. Tambwe***  
***MBEYA***  
***19 - 20/06/1968***

---